# BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA

# MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU

# KIDATO CHA PILI

# ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

# MWONGOZO WA USAHIHISHAJI JULAI/AGOSTI, 2026

Shulelibrary.com

## SEHEMU A (Alama 15)

1.

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | A | C | A | B | D | C | A | D | B |

**Alama 01 @ swali = Alama 10**

2.

| ORODHA A | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| ORODHA B | C | E | A | G | D |

**Alama 01 @ swaliu = Alama 05**

## SEHEMU B (Alama 70)

3. Wajibu wa mke kwa mumewe:

(i) Kumtii mumewe katika yale yote mema anayoamrishwa naye, kwani kufanya hivyo katika kumtii Allah.

(ii) Kumfurahisha na kumliwaza mumewe kama alivyokuwa Bi Khadija kwa Mtume (S.A.W)

(iii) Kulinda heshima na mali ya mume, hapaswi kufanya chochote isipokuwa kwa ruhusa ya mumewe.

(iv) Kumvumilia mumewe kwani kufanya hivi kunasaidia kuepusha migogoro mikubwa ndani ya ndoa.

(v) Kutosheka na alicho nacho mumewe

(vi) Kutunza siri ya mumewe

(vii) Kumkumbusha mumewe kheri

**Dondoo nne (4) @ 02 ½ = alama 10**

4. Hekima ya Qurán kushushwa kidogo kidogo:

(i) Kumsaidia Mtume (S.A.W) kufikisha kikamilifu kinadharia na kivitendo.

(ii) Kuimarisha moyo wa Mtume (S.A.W) na Waislamu wa mwanzo, hasa katika kile kipindi kigumu cha upinzani dhidi ya Washirikina wa Makkah.

(iii) Kuwawezesha kuelewa, kuhifadhi na kutekeleza mafundisho ya Qur'an kwa wepesi.

(iv) Kutoa majibu ya maswali na kueleza kwa matukio ya wakati uliopo.

(v) Kuthibitisha kuwa Qurán ni kitabu cha Allah (S.A.W), kwani kwa kawaida wanadamu hutoa maandiko yao baada ya kukamilika kabisa.

**Dondoo nne (04) @ 02 ½ = Alama 10**

5. Sifa za ujumbe unaopaswa kulinganiwa kwa watu.

(i) Utokanae na Qurán na Hadithi sahihi za Mtume (S.A.W)

(ii) Uwe unamwezesha mtu kuitambua hadhi yake katika jamii Pamoja na lengo lake la kuumbwa.

(iii) Umjenge msikilizaji na kumpa hamasa ya kuufuata Uislamu katika kila kipengele cha Maisha yake.

(iv) Umwezeshe mtu kuwa na mtazamo sahihi wa Uislamu kwa kufuata Qurán na sunnah.

(v) Uepukane na aina zote za laghawi, kama vile hadithi za "paukwa pakawa", kwani humfanya msikilizaji kuishia kucheka na kutozingatia maudhui inayokusudiwa.

(vi) Utolewe kwa kuzingatia lugha ya msikilizaji ilia pate kuelewa kwa usahihi.

**Dondoo tano (05) @ 02 = 10**

6. Mafunzo yatokanayo na mbinu za kulingania alizozitumia Nabii Ibrahim (A.S).

(i) Mlinganizi wa Dini ya Allah anapaswa kuwa mfano wa kuigwa katika kila kipengele cha Maisha yake.

(ii) Daáwa huanza kufanywa kwa wa karibu.

(iii) Walinganizi wanaaswa kuanza kulingania upweke wa Allah kabla ya mengineyo.

(iv) Walinganizi wanapaswa kutumia hoja zenye mashiko ili kuondoa wasiwasi kwa wanaolinganiwa.

(v) Ujasiri ni nyenzo muhimu sana katika kulingnia Uislamu/ kutomuogopa mto yeyote

Shulelibrary.com

(vi) Kuwa na vituo maalumu kwa ajili ya kazi ya ulinganizi ni jambo muhimu.

(vii) Subra na uvumilivyo huleta athari Chanya katika daáwa.

(viii) Kutumia lugha ya upole

**Dondoo tano (05) @ 02 = 10**

7. (a) Madai ya makafiri juu ya uwepo wa Allah (S.W)

(i) Allah hayupo kwa sababu haonekani

(ii) Mwanadamu ndiye aliyefanya kuwepo kwa Allah kutokana na kushindwa kwake kutatua changamoto zake.

(iii) Nasaha ya Allah (S.W) haijulikani

(iv) Hapana Allah Muumba kwani vitu vyote vimezuka tun a vitatoweka muda ukifika.

**Hoja mbili (02) @ 02 ½ = 05**

(b) Udhaifu wa hoja za makafiri juu ya uwepo wa Allah kama ilivyo katika kipengele cha (a).

(i) Milango ya fahamu ina udhaifu mkubwa, kwani kuna wakati inatoa majibu yasiyo sahihi.

Si kila kisichoonekana hakipo, mfano upepo, akili n.k

(ii) Hakuna uthibitisho wa kihistoria kuwa mwanadamu alianza Maisha akiwa na fikra duni.

(iii) Muumba ndiye chanzo na asili ya vitu vyote, hivvyo hawezi kuwa na nasaba, mwanzo wala mwisho. (Rejea Qurán Al-Ikhlas: 1-4)

(iv) Haiwezekani kkuwepo kwa jambp Fulani au kitu kisha asiwepo aliyekifanya kitu hicho kuwepo. Mfano iwepo nyumba na asiwepo mjengaji.

**Hoja mbili (02) @ 02 ½ = 05 Jumla alama 10**

8. Faida anazozipata mja anayeanza mambo yake mema kwa "Bismillah"

(i) Kupata msaada na baraka za Allah katika jambo lake

(ii) Kujikinga na kufanya maovu/ kujikimga na shetani

Shulelibrary.com

(iii) Humzoesha kuwa na tabia ya kumkumbuka na kumtaja Allah

(iv) Humfanya kubakia katika utii wa Allah na ibada zake.

**Dondoo nne (04) @ 02 ½ = 10**

9. (a) (i) Maana ya kuchunga ahadi

Ni kutekeleza au kutimiza ahadi za lazima za Allah s.w) na zile tunazowekeana wanadamu wenyewe kwa wenyewe.

(ii) Uaminifu ni:

Ni hali ya kuchunga amana mbalimbali ulizokabidhiwa na Allaj (S.W) na zile ulizokabidhiwa na wanadamu wenzio.

**@ 02 = 04**

(b) Faida za uaminifu katika jamii

(i) Huleta amani na usalama

(ii) Hukuza maendeleo ya Uchumi wa mwanadamu

(iii) Huleta mapenzi na ushirikiano baina ya wanajamii

**Dondoo tatu (03) @ 02 = 06**

**JUMLA ALAMA 10**

Shulelibrary.com

10. Umuhimu wa ibada ya funga ya Ramadhani

(i) Funga ni faradhi kwa waumini wote.

Kila Muislamu aliyekidhi sifa zote stahiki anapaswa kutekeleza ibadah ii bila ya visingizio vyovyote, kwani kama mtu hatofanya hivyo hupelekea kupata adhabu ya Allah kwa kutotekeleza amri ya Allah kwa wanadamu wote. Kuonesha umuhimu huo, yeyote mwenye dharura isiyo ya kudumu hupaswa kulipia funga zote alizoziacha wakati wa dharura. Mfano safari au ugonjwa. Hivyo binti huyu amuogopa Allah na adhabu zake, kwani hamkomoi mtu anajikomoa mwenyewe.

(ii) Funga ya Ramadhani ni nguzo ya nne ya Uislamu

Hivyo, hata mja akiwa mtekelezaji wa nguzo zote za Uislamu na akaacha funga kwa makusudi basi Uislamu wake unakuwa haujatimia, pia anajifananisha na wale waliotajwa vibaya na Allah kuwa wanaamini baadhi ya amri na wanazikufuru nyingine. Hivyo, binti huyu ajiondoe katika kundi hili la watu waovu.

(iii) Funga ina malipo makubwa mbele ya Allah

Allah ameipa hadhi ya kipekee ibadah ii kwa kuinasibisha na yeye mwenyewe naye ndiye mwenye kuilipa. Pia ameweka mlango maalumu peponi kwa ajili ya wafungaji. Hivyo ni vema binti huyu ayajue hay ana ayafanyie kazi ilia pate malipo hayo makubwa.

(iv) Fung ani miongoni mwa ibada zitakazomuombea mja siku ya Qiyama

Miongoni mwa ibada zilizopewa nafasi maalumu ya kuwaombea watendaji wake ni funga, hivyo, yeyote atakayekuwa mbai na ibadah ii huikosa ofa hii na si hivyo tu, bali huweza kuwa na sababu ya mja huyo kutoingia peponi.

(v) Funga ya Ramadhani hupelekea mja kusamehewa madhambi yake na kuwekwa mbali na moto

Kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu, ndani ya mwezi wa Ramadhani kila usiku Allah huwasamehe waja wake na kuwatoa motoni, pia atakayesimama katika kisimamo cha Ramadhani kwa Imani sahihi na matarajio mema kwa Allah, husamehewa maduambi yake yaliyotangulia.

Hivyo, ni hasara iliyoje kwa Muislamu anayepuuza nguzo hii muhimu, kwani ia anayeitekeleza vilivyo nguzo hii ni dhahili anakuwa anaukaribia ucha Mungu.

(vi) Funga ni kitambulisho cha muislamu wa kweli

(vii) Funga humfanya mtu kuwa mkarimu

**Utangulizi: 01 ½**

**Kiini: Hoja nne (04) # 02 = 12**

Shulelibrary.com

**Hitimisho: 01 ½**

**JUMLA: 15**

Shulelibrary.com